**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

# KUHUSU UZINDUZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA, 2026

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima, afya njema na kutukutanisha hapa leo. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha na kuwashukuru kwa kuitikia wito wa kuhudhuria mkutano huu muhimu wa vyombo vya habari. Kupitia mkutano huu, napenda kuwataarifu wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya maandalizi ya uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2026 yaliyofikiwa na dhima ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu kwa ujumla.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2026 zitazinduliwa rasmi tarehe 02 Aprili 2026 kuanzia saa 1.00 asubuhi katika uwanja wa Mpira wa Miguu wa Gombani, uliopo katika Wilaya ya Chake chake Kusini Pemba.

Mgeni Rasmi katika tukio hili atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Maandalizi yote kwa ajili ya sherehe za uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru yameshakamilika na vijana shupavu walioteuliwa kwa ajili ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru nchini wapo tayari kwa kazi hii ya kizalendo ya siku 195.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Mwenge wa Uhuru ni Tunu ya Taifa tuliyoachiwa na waasisi wa Taifa letu ambayo falsafa yake ndiyo inayobeba misingi ya uhai wa Taifa la Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake hadi leo, Mwenge wa Uhuru umeendelea kuhamasisha wananchi kuishi kwa kuzingatia misingi ya amani, umoja wa kitaifa, haki, usawa, uwajibikaji kwa jamii na uchapaji kazi kwa maendeleo ya Taifa.

Falsafa ya Mwenge wa Uhuru iliasisiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Mwaka 1961 na kuungwa mkono na muasisi wa Taifa la Zanzibar Sheikh Abeidi Aman Karume pale aliposisitiza juu ya wananchi kumiliki njia kuu za uchumi, uimarishaji wa huduma za kijamii, umiliki wa ardhi na ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo. Aidha, tarehe 26 Juni, 1964 Mbio za Mwenge wa Uhuru zilianza rasmi nchini kwa misingi ile ile iliyojipambanua katika falsafa yake, ajenda kuu ikiwa kulinda uhuru, kulinda mapinduzi matukufu ya zanzibar,kulinda Muungano wetu, kujenga Taifa huku nuru ya Mwenge wa Uhuru ikiendelea kuiangaza Afrika na dunia juu ya

ukombozi wa mtu mweusi na binadamu wote popote pale duniani dhidi ya unyonyaji, ukatili na ubaguzi

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Kila Mwenge wa Uhuru unapokimbizwa huambatana na ujumbe maalumu kwa wananchi ambao hutoa dira na mwelekeo wa Taifa kwa wakati huo. Kwa mwaka 2026, ujumbe mkuu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru umejielekeza katika kuhamasisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa chini ya Kauli Mbiu inayosema:- ***"Tanzania ni Yetu Sote, Tushikamane kwa Pamoja Kuleta Maendeleo."***

Kauli mbiu hii inalenga kuwakumbusha wananchi juu ya umuhimu wa amani katika ujenzi wa Taifa na kuwataka Watanzania kuendelea kulinda amani ya nchi yetu, kudumisha umoja wetu na kuimarisha mshikamano miongoni mwa Watanzania.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2026, wananchi wa Tanzania wataendelea kuelimishwa na kuhamasishwa kuendeleza mapambano dhidhi ya VVU/UKIMWI, Rushwa, Dawa za Kulevya, Malaria na uzingatiaji wa Lishe bora kwa afya imara.

Aidha, katika kuwapa vijana wetu fursa ya kusikilizwa na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Taifa, Serikali kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru itaendelea kuimarisha ushiriki wa vijana katika

shughuli za maendeleo ya Taifa kupitia majukwaa ya Vijana (Youth platforms) katika ngazi za Halmashauri nchini.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Majukwaa haya ya vijana katika ngazi ya Halmashauri na Mikoa ninayoyazindua yatawawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika maamuzi ya maendeleo ya jamii zao, kupata taarifa kuhusu fursa za ajira na uwezeshaji na kwa kushirikiana na wataalamu waliopo katika maeneo yao watajengewa uwezo wa kijasiriamali, ubunifu na mitaji. Majukwaa haya pia ni fursa ya kujenga misingi ya umoja na uzalendo kwa vijana lakini pia ni kielelezo cha utawala unaowajibika kwa watu wake. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuwahimiza viongozi wa Mikoa na Halmashauri zote nchini kuhakikisha majukwaa haya ya vijana yanaanzishwa na kuendeshwa kwa ufanisi ili yawe chachu ya maendeleo katika maeneo yao na Mwenge wa Uhuru pamoja na majukumu mengine utatumika kuzindua rasmi majukwaa haya kila Halmashauri kwa utaratibu uliotolewa katika Vigezo vya Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2026.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Baada ya uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru tarehe 02 Aprili, 2026 Mkoani Kusini Pemba, Mwenge wa Uhuru utakimbizwa katika Mikoa yote 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Halmashauri zote 195 na zitafikia kilele chake tarehe 14 Oktoba, 2026 Mkoani Rukwa. Kwa kipindi hiki cha siku 195, Mwenge wa Uhuru utapita katika

maeneo mbalimbali ya nchi yetu ukihimiza amani, upendo na mshikamano wa kitaifa kwa watanzania. Aidha, utafanya kazi ya Kutembelea, kukagua, kufungua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo nchini kote. Kazi hii itakwenda sambamba na kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuendelea kupambana na adui rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Ninaomba kutumia fursa hii kuwaalika wananchi Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Zanzibar na Watanzania wote kujitokeza kwa wingi kushiriki kwenye uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2026 utakaofanyika tarehe 02 Aprili 2026 katika Uwanja wa Gombani kuanzia saa 1.00 asubuhi na kwa pamoja *tushuhudie* Mheshimiwa Dkt.Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akiwasha na kuukakabidhi Mwenge wa Uhuru kwa vijana wetu shupavu walioandaliwa kuukimbiza katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimalizie kwa kusema **“Tanzania ni Yetu Sote, Tushikamane kwa Pamoja Kuleta Maendeleo**.”

Mwenge wa Uhuru Oyeee......

Ahsanteni kwa kunisikilza

DKT. JOEL ARTHUR NANAUKA (MB)
**WAZIRI WA NCHI**
**OFISI YA RAIS – MAENDELEO YA VIJANA**